

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



## TAARIFA KWA UMMA.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni Ndugu Aron T. Kagurumjuli kwa niaba ya Timu ya menejimenti na Baraza la Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni leo amewapongeza Wanafunzi, Walimu, viongozi wa shule za msingi na wazazi kwa kuwezesha kupata matokeo mazuri ya kumaliza elimu ya msingi darasa la saba mwaka 2017 kwa kufaulisha watoto kwa asilimia 93.02% na kushika nafasi ya kwanza kitaifa.

Kwa mujibu wa matokeo yaliyotangazwa na baraza la mitihani la Taifa, Manispaa ya Kinondoni imeshika nafasi ya kwanza kitaifa na Kimkoa kati ya shule 188 ambapo kiwango cha ufaulu wa Manispaa kimepanda kwa kutoka nafasi ya 11 kati ya shule 181 kwa ufaulu wastani wa asilimia 84.4 % na kuwa nafasi ya 1 kati ya shule 188 kwa ufaulu wa asilimia 93.02 mwaka huu 2017 sawa na ongezeko la karibuasilimia 9% ambalo kimsingi ni mafanikio makubwa na ya kihistoria.

Kwa kutambua mafanikio haya uongozi wa Manispaa na Wilaya ya Kinondoni leo umetoa tuzo katika makundi mbalimbali kama ifuatavyo:-

- ❖ Tuzo kwa walimu wakuu ambao shule zao zina ufaulu wa juu zaidi kwa shule 78 zilizopo Manispaa ya Kinondoni
- ❖ Tuzo kwa shule zilizokuwa na mabadiliko makubwa katika ufaulu kwa shule 10 za Manispaa ya Kinondoni.
- ❖ Tuzo kwa walimu waliofundisha kikamilifu na kwa weledi na kutoa daraja A nyingi katika shule zao .
- ❖ Tuzo kwa Kata zilizofanya vizuri zaidi kwa kata tatu za Makumbusho , Msasani na Magomeni.

Wakiwa katika hafla ya kutoa tuzo hizo leo katika shule ya msingi Mbuyuni Kata ya Msasani kauli iliyotawala kwa kila kiongozi akiwemo Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni , Mhe Alli Happi, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni Mhe. Benjamini Kawe Sitta , Mwenyekiti wa kamati ya Huduma za uchumi Afya na Elimu Mhe. Thadei Masawe na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni Ndugu Aron T.Kagurumjuli ni kuwa “Nawapongeza sana Wanafunzi, Walimu, Kamati za

shule na Wazazi na idara ya elimu ya msingi kwa ushirikiano na mshikamano wa kuhakikisha Manispaa ya Kinondoni inaendelea kufanya vizuri kitaaluma na ninawatakia maandalizi mema wazazi na walezi wa wanafunzi waliofaulu na ninawataka wote wajiunge kidato cha kwanza Januari 2018" alisisitiza kila kiongozi aliyezungumza katika hafla hiyo.

Mwisho Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mhe Alli Hapi ameziagiza Kata zote kuanza kampeni ya maandalizi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule zote ili kuondoa changamoto inayoikabili Manispaa ya Kinondoni ya upungufu wa vyumba 112 vya madarasa. Kisha akawatakia maandalizi mema ya mafanikio zaidi katika mtihani ujao na kwamba Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kwa kushirikiana na serikali kuu na wadau wengine itaendelea kushughulikia changamoto zote za sekta ya elimu ili kuwa na mazingira bora yatakayoweza kufanikisha adhima yetu ya kuendeleza mafanikio haya.

Imetolewa na:-



Sebastian M. Mhowera

**AFISA UHUSIANO WA MANISPAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI.**